**Title: Under the Mango Trees**

**EPISODE 5**

**Author: Romie Singh**

**Editors: Susanne Fuchs, Katrin Ogunsade, Maja Braun**

**List of characters for episode 5:**

- Narrator
- Desirée
- Endurance
- Lorraine
- Sazi
- Bella
- Bongo
- Children in background

Karibu kwenye sehemu ya tano ya Noa Bongo Jenga maisha Yako katika mchezo kwa jina Chini ya Miembe.Mchezo unaojadili njia za kupanga uzazi.  Leo hii, Lorraine anashangaa kipi kinacho endelea kati ya kaka yaake Eric na rafiki yake mpendwa Desirée. Lorraine, mwenyewe na mpenzi wake Sazi, wanaendelea vizuri na maisha yao, wanazungumza bila hofu juu ya maswala mbali mbali pamoja na mpango wa uzazi. Wakati huo huo, Desirée nae afahamu mengi kutoka kwa dada yake Bella, kuhusu  uamuzi wake wa kutopata mtoto sasa. Karibu ili upate yote yanayo endelea katika mchezo huu wa kusisimua!

**SIG.TUNE UP HOLD UNDER AND FADE**

1. **SFX: Wind**

**NARRATOR:** Mtelera ni kijiji kidogo, upepo mkali unavuma, vumbi kutoka mashambani linamfanya Endurance akohoe zaidi kuliko kawaida. Desirée ameamka mapema kumchemshia kinywaji cha moto.

**Sc. 1 In the kitchen. Early morning ambience**

2. **SFX:** chickens etc., children playing around, laughing etc.

3. **SFX:** Endurance coughing

4. DESIRÉE: Shika, Endurance. Kunywa ni mizizi iliyochemshwa.

5. ENDURANCE: (Sipping tea) Nilifurahi sana tulipowatembelea kina Eric. Juisi ya maembe ya Aunty Alice niliipenda sana, na wewe je? Kwanza na vibonge vya barafu!

6. DESIRÉE: (dreamily) Ndio ilikuwa tamu... nzuri sana.

7. ENDURANCE: kule na utulivu, kulikuwa kimya sio kama hapa tupo watoto wengi katika nyumba ndogo. Kwani mjomba Blessing atakuja lini kuwachukua watoto wake?

8. DESIRÉE: Hata sina hakika, kwa kweli mimi ningependa niwe na chumba changu!

9. ENDURANCE: hata mimi!Lakini kwanini Aunty Alice ana watoto wawili tu? Au alipata ugonjwa baada ya kuzaa hao mapacha? Labda alilaaniwa , unajua, Des?

10. DESIRÉE: Hapana, haiwezekani. Natumai siku hizo zimepitwa na wakati ambapo watu waliamini kuwa kupata mapacha ni laana! Aunty na Uncle Joshua walipanga kuwa na familia ndogo. Walitaka kuendelea na kazi yao ya udaktari. Kwa hivyo walipopata watoto wawili kwa mara moja hiyo iliwarahisishia kazi. Aunty Alice aliweza kuwatunza watoto na kuendelea na kazi baada ya muda mfupi tu..

11. **SFX:** Endurance starts coughing.

Haya! Kunywa basi wakati bado ni moto.

12. ENDURANCE: (sipping) Ndio maana, wanaishi kwenye nyumba nzuri. Lakini Eric alisema anatamani kama angekuwa na ndugu zaidi, alisema anajihisi mpweke mara nyingine. Alinionyesha vitabu vyake vya udaktari. Nakwambia ana mabaki ya

mifupa ya mwanadamu chumbani mwake! Sikulala! Nilidhani mabaki hayo yatageuka mtu usiku anikamate, lo!

13. DESIRÉE: (laughing) Hiyo ni mifupa tu, mjinga wee! Sasa nafikiri ungeamka ujitayarishe kwa ajili ya kwenda shule.

14. MUSIC UP

**NARRATOR:** Shuleni, Desirée alijiunga na Lorraine kabla masomo hayaja anza.

**Scene 2 At school**

15. **SFX**: School break, people talking, laughing etc. In background

16. LORRAINE: Ulimfanyaje kaka yangu? Alikuja nyumbani kuchelewa jana na macho yake yalimeremeta!

17. DESIRÉE: (laughing) Lorraine, wewe una WAZIMU!

18. LORRAINE: Najua. Sawa basi utaniambia wakati mwingine kwanza tuimbe wimbo mmoja kabla ya kwenda darasani.

19. **SFX**: Lorraine and DESIRÉE sing a new song, laughing, improvising, making mistakes

20. **SFX**: School bell ringing

21. DESIRÉE: Oh, sasa – lazima tuondoke. Je hatuwezi kuimba baada ya masomo?

22. LORRAINE: (happily excited) Pole, rafiki yangu, mimi nina miadi na mpenzi wangu Sazi baada ya masomo!

**NARRATOR:** Sazi ana miaka 19 na anasomea upishi katika chuo cha mji wa Kentown. Alipendendelea kuzungumza juu ya ndoto na malengo yake pamoja na mpenzi wake, Lorraine. Kila uamuzi waliupitisha pamoja. Hata matumizi ya dawa za kuzuia uzazi waliamua pamoja. Kwa nini asumbuliwe peke yake na wazo la kupata mimbat? Bila shaka Sazi alikuwa tayari kusikiliza mipango ya mpenzi wake hasa baada ya kukutana na Bongo.

**<u>Scene 3 Interior.</u>**

23. **SFX:** Soft music in the background

24. SAZI: Enhe? unadhani Bongo anafikiri kuwa wewe una nafasi nzuri?

25. LORRAINE: Nafikiri. Aliipenda sana sauti ya Desirée pia.

26. SAZI: Na wewe? Itakuwaje ukishinda?

27. LORRAINE: nitapaa mwezini nakwambia! Itategemea watu watakavyo piga kura, kuanzia wale watakaofika kwenye tamasha na wale watakaokuwa wanaangalia kwenye Televisheni. Najua haitakuwa rahisi kushinda.

28. SAZI: TV! Wow, Lorraine! Utakuwa nyota! Nitawaambia jamaa zangu wote pamoja na maraafiki zangu wakupigie kura! Hebu njoo karibu nami unaruka ruka kama panzi! Kwani sitakupata tena kukupa busu?

29. LORRAINE : (kissing) Utanipata! Oh, utanipata!

30. SAZI: (softly) Natumai utaendelea kuzungumza na mimi hata baada ya kuwa mtu maarufu.

31. LORRAINE: (softly) Usiseme hivyo. Nisingefanya haya yote bila ya usaidizi wako.

32. SAZI: (kissing) Kwa hivyo nisiwe na wasiwasi wa kunyang'anywa?

33. LORRAINE: Usiwe na wasiwasi! nakupenda.

34. SAZI: (kissing) Hmmm. Je unaendelea kutumia tembe zako? Bado una kinga?

35. LORRAINE: (kissing) Ndio, Sazi. Niko salama...

36. **SFX:** Intimate sounds of breathing and kissing.

37. MUSIC UP

**NARRATOR:** Dada mkubwa wa Desirée, Bella, aliwatunza watoto wikiendi ilizopita wakati Desirée na Endurance walipokwenda kwa Lorraine na kuamua kukaa siku moja zaidi. Mpenzi wake, Robert, alikwenda kutembea na marafiki zake, Bella hakupenda kubaki peke yake. Alifurahi kuwa na watoto nyumbani, lakini kwa nini hataki kuwa kuwa na mtoto yeye mwenyewe? Desirée ameamua kumuuliza.

**<u>Scene 4 In the kitchen.</u>**

38. **SFX:** washing up.

39. BELLA: Eti kwa nini? Kwa sababu mimi bado ni mdogo. Hatuwezi kupata mtoto wakati mimi nataka kukamilisha masomo yangu kisha nataka nifanye kazi kabla ya kupata mtoto. Kwa nini umeuliza lakini? Au nyanya amekuwa akisema?

| | | |
|---|---|---|
| 40. | DESIRÉE: | hapana. Nilitaka kujua tu basi. |
| 41. | BELLA: | Angalia Des, wewe ni msichana mkubwa na unapaswa kujua kuhusu mambo haya. Sio siri siku hizi. Mwanamke ana uhuru wa kuchagua ni wakati gani anataka kupata mtoto. Mama yetu hakudhani kama angeweza kujichagulia. |
| 42. | DESIRÉE: | Nakumbuka nyanya aliwapeleka yeye na baba kwa mganga wa kienyeji eti mama akapewe dawa ya kumfunga uzazi. |
| 43. | BELLA: | Ndio, Nakumbuka pia mimi. Tena matibabu hayo yalimpa maumivu makali na mwishowe akapata mimba hivyo hivyo halafu ikatoka. (Clicking her tongue) Ai! Ninapenda jinsi Aunty Alice anavyo eleza kuhusu njia tafauti ambazo mwanamke anaweza kuzitumia. Alimweleza mama kuwa angeweza kufunga uzazi au angetumia Koili. Koili au IUD kwa kimombo anawekewa mwanamke ili kuzuia asipate mimba. Huwa inatoa Homoni kuzuia rutuba katika yai lakini hii ni tafauti na tembe maanake huna wasiwasi wa kufikiria kumeza kila siku. |

44. DESIRÉE: Bila shaka Nyanya alipinga njia zote hizo?.

45. BELLA: (whispering angrily) Kwani unafikiria ni kwa nini mimi niliamua kuhama kutoka hapa nyumbani. Ni wazi kuwa nyanya anapinga njia zote za kupanga uzazi. Lakini najua mama yetu angekuwa hai mpaka leo iwapo angefanyiwa operesheni ndogo tu tena bure katika hospitali ya taifa, hilo tu ndilo alihitaji. Daktari Alice angeifunga mirija yake kuzuia asipate uja uzito. Je unaelewa ninachosema, Des?

46. DESIRÉE: Nafikiri naelewa. Unazungumzia kuhusu kukata uzazi, si ndio?

47. BELLA: (laughing) Hapana! Mwanaume ndio hufanya operesheni kama hiyo anapo amua kuwa hataki watoto tena.’ Mwanamke anafungwa tu mirija yake ili mayai ya uzazi yasiweze tena kwenda kwenye kizazi, na manii hayawezi kukutana na mayai hayo. Na hatua hiyo hua ni ya kufunga kizazi moja kwa moja.

48. DESIRÉE: Kwa hivyo lazima uwe na hakika kuwa hutaki tena watoto.

49. BELLA: Haswa. Au labda uwe umeshapata watoto wa kutosha na hutaki tena kuongeza mtoto mwingine pengine hata mwili wako ukiwa umechoka hauna nguvu tena ya kupata watoto zaidi.

50. DESIRÉE: Hayo ni maamuzi makubwa.

51. BELLA: Ni kweli lakini uamuzi huo ni rahisi kwa wanawake wa makamo, na pia katika desturi zingine mwanamke akisha kuwa nyanya basi anatarajiwa kuacha kuendelea kuzaa. Ndio maana wanawake wengi wa makamo wanakata uzazi kabisa. Lakini hatua kama hiyo inaweza kufanyiwa mama ambae maisha labda yanaweza kuwa hatarini kwa kupata mimba nyingine na mama yetu alikuwa kwenye fungu hilo. Inanisikitisha sana.

52. **SFX** Cell ring tone keeps ringing. SFX Feet running. Door opens.

53. ENDURANCE: (out of breath) Simu ina! Des ni ya nani?

54. BELLA: Hee. tangu lini mna simu ya mkononi nyie?

55. DESIRÉE: (excited) Shhh, nyamazeni nyote.

56. ENDURANCE: (silly voice) Au ni mpenzi wako Eric?

57. DESIRÉE: (hissing angrily) Shhh. Endurance. Unaweza kutoka nje tafadhali?

58. BELLA: Eric? Ooh, kitu gani kinaendelea mdogo wangu?

59. DESIRÉE: (excited) Nitakwambia baadae wacha kwanza nijibu simu hii.

60. ENDURANCE: Kama ni Eric ninataka kuzungumza nae.

61. DESIRÉE : Shhh.

62. *SFX:* Cell ring stops

Um… hallo? (Louder) Ndio, hallo?

63. BONGO: (telephone voice) Desirée? Ni mimi, Bongo. Hujambo?

64. DESIRÉE: (confused) Bongo?... Oh! Bongo! Um... sijambo sijui wewe?

65. BONGO: Salama tu. Nina habari nzuri. Kwako. Unanielewa?

66. DESIRÉE: (still confused) Er, Unasemaje?

67. BONGO: nakwamabia usimwambie mtu habari hizi, tena hasa Lorraine. Usimwambie kwanza. SAWA?

68. **SFX:** Cell phone line goes dead

69. DESIRÉE: Bongo? (shouting louder) Bongo? Oh simu imekatika.

70. SIG TUNE UP

**OUTRO:**

Asante kwa kusikiliza Noa Bongo Jenga maisha Yako. Ni hayo tu kwa leo katika mchezo wa kusisimua kwa jina Chini Ya Miembe. Jiunge nasi katika sehemu ya sita wiki ijazo wakati ambapo Desirée anakabiliwa na wakati mgumu. Je achukue nafasi ya kuimba au aendelee kuwalea watoto wa mjomba wake alio waacha?.

Kumbuka ukitaka kuusikiliza tena mchezo huu au kumwambia rafiki yako ausikilize basi sikiliza katika mtandao na anuwani yetu ni d w world dot d e mkwaju l b e

Hadi wakati mwingine. Kwaheri.

END OF EPISODE FIVE